



# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



## Hatua za awali za Ujenzi wa Zahanati katika mtaa wa Nyambiti Kata ya Buzuruga



### Habari kwa Ufupi

Mhe. Hasan Masala, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na wataalam na kushiriki pamoja na wananchi wa Mtaa wa Nyambiti kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati katika Mtaa huo

Mhe. Masala, Amewapongeza wananchi hao kwa michango yao waliyotoa na amesisitiza suala la uadilifu katika michango ya wananchi na kuelekeza kuwa taarifa ya mapato na matumizi ya michango hiyo iwekwe wazi kwa wananchi.

Nae Mhe. Manusura Lusigaliye Diwani wa Kata ya Buzuruga amemshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuunga juhudi hizo na kusema kuwa zahanati hiyo ilikuwa ni hitaji la muda mrefu kwa wananchi wa mtaa wa Nyambiti.

Wananchi wa mtaa huo kwa umoja wao wamechangia saruji mifuko 120. trip 30 za mawe, mchanga trip 8, huku Umoja wa mafundi wa Kata ya Buzuruga wamechangia kwa kuchimba msingi zahanati hiyo



*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga  
Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*